**TANGAZO LA SERIKALI Na....... lililochapishwa tarehe...../........../2021**

SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA TANZANIA
(SURA 219)

## KANUNI

*(Zimetengezwa chini ya kifungu cha 122 (1) (i))*

# KANUNI ZA ADA NA TOZO ZA DAWA NA VIFAA TIBA, 2021

MPANGILIO WA KANUNI


1. Jina
2. Matumizi
3. Tafsiri

SEHEMU YA PILI
ADA NA TOZO

4. Ada na tozo
5. Matumizi ya ada na tozo
6. Malipo kwa amri ya mahakama
7. Ada na tozo zilizoainishwa kwenye kanuni nyingine
8. Ada za ukaguzi wa viwanda
9. Ada ya bidhaa za matangazo
10. Ada za bidhaa za tumbaku

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA JUMLA

11. Makosa na adhabu
12. Kufifilisha makosa
13. Kufutwa na kuhifadhi

**MAJEDWALI**

**TANGAZO LA SERIKALI NA....... lililochapishwa tarehe...../........../2021**

SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA TANZANIA
(SURA 219)

**KANUNI**

*(Zimetengezwa chini ya kifungu cha 122 (1) (i))*

KANUNI ZA ADA NA TOZO ZA DAWA NA VIFAA TIBA, 2021

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ada na Tozo za Dawa na Vifaa Tiba za mwaka 2021.

Matumizi

**2.** Kanuni hizi zitatumika katika kutoza ada kwa ajili ya udhibiti wa bidhaa ikiwa ni pamoja na dawa, vifaa tiba, vitendanishi, vifaa vya maabara, damu na mazao yake, gesi tiba, vipukusi, bidhaa za tumbaku, bidhaa zisizodhibitiwa na bidhaa nyingine zinazohusiana na tiba ndani ya Tanzania Bara.

Tafsiri

**3.** Katika Kanuni hizi Isipokuwa muktadha utahitaji vinginevyo:

Sura 219

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba;
"ithibati" maana yake ni utambuzi rasmi wa maabara za afya za umma na binafsi ili kubaini kama zinakidhi viwango vya kimataifa;
"ada ya mabadiliko" maana yake ni ada inayolipwa na mmiliki wa bidhaa pale anapoomba mabadiliko ya viambata, vifungashio, taarifa kwenye lebo au mabadiliko mengine yeyote ya bidhaa iliyosajiliwa;
"sampuli za mnyama za kibaiolojia" maana yake ni sampuli zinazochukuliwa kutoka kwa mnyama kama vile damu, mkojo, mnofu, viungo, mate, ute wa uti wa mgongo, manyoya, kucha au sampuli yoyote inayotokana na mnyama;
"ada ya mwaka ya kushikilia bidhaa" maana yake ni ada inayolipwa kwa mwaka na mmilki wa bidhaa kwa ajili ya kushikilia usajili katika rejista ya usajili wa bidhaa ya Mamlaka;
"viua vimelea vya ngozi na utando" maana yake ni bidhaa zinazotumika kwenye ngozi au utando telezi ili kuua, kupunguza au kuzuia ukuaji wa vimelea vya magonjwa;
"vipukusi"; maana yake ni viua vimelea vya ngozi, utando telezi, mazingira na vifaa tiba;
"bei elekezi" maana yake ni bei iliyowekwa na Mamlaka kwa ajili ya dawa

kwa mujibu wa Kanuni za Bei Elekezi za Mamlaka;

“gharama za mzigo na usafirishaji” maana yake ni gharama za mzigo, usafirishaji pamoja na bima ya mzigo;

“sampuli za kibiashara” maana yake ni sampuli zinazowasilishwa na mteja nje ya utaratibu wa usajili kwa ajili ya upimaji;

“mteja” maana yake ni mtu yeyote anayepokea huduma za Mamlaka;

“viua vimelea vya mazingira” maana yake ni bidhaa zinazotumika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa lengo la kuua vimelea kwenye mazingira na vifaa tiba;

“kuondoa au kuharibu” maana yake ni kitendo cha kugawa sampuli au bidhaa zinazofaa au kuteketeza zisizofaa kwa matumizi ya binadamu;

“bidhaa za ndani” maana yake ni bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani ya Tanzania Bara;

“bidhaa za msaada” maana yake ni dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotolewa kwa msaada na taasisi zinazotambulika na Mamlaka isipokuwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotolewa kupitia miradi msonge;

“ada” maana yake ni gharama yoyote inayolipwa kwa lengo la kupata huduma za Mamlaka;

TS. Na. 295

“gharama za mzigo” maana yake ni thamani ya mzigo unaodhibitiwa na Mamlaka unaokusudiwa kuingizwa Tanzania Bara;

“utengenezaji bora wa bidhaa” maana yake ni mifumo na taratibu zilizoainishwa kwenye Kanuni za Utengenezaji Bora wa Dawa za mwaka 2018;

"bidhaa zinazoagizwa nchini" maana yake ni bidhaa zilizotengenezwa nje ya Tanzania Bara;

Sura ya 287 na 288

“bidhaa ya uvumbuzi” maana yake ni bidhaa yenye haki miliki ambayo imeidhinishwa kwa mara ya kwanza kupita tathmini ya ubora, usalama na ufanisi na kuthibitishwa matumizi yake kwa binadamu:

Sura 219

“viwanda vikubwa” maana yake ni viwanda vyenye mtaji wa uwekezaji unaozidi shilingi za kitanzania milioni mia nane;

Sura 219

“mamlaka ya serikali za mitaa” maana yake ni mamlaka za mikoa na wilaya kama zilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Mamlaka za Wilaya za Serikali za Mitaa na Sheria ya Mamlaka za Miji za Serikali za Mitaa;

“mtengenezaji” maana yake ni mtu au kampuni inayotengeneza bidhaa zinazodhibitiwa chini ya Sheria;

“utengenezaji” maana yake ni taratibu zote zinazohusika katika kuandaa, kuchakata, kujaza, kuboresha, kuchanganya, kupaki na kuweka lebo kwenye bidhaa zinazodhibitiwa chini ya Sheria;

"mmiliki wa idhini ya uuzaji" maana yake ni kampuni au shirika ambalo limepewa idhini ya uuzaji ambayo inaruhusu mmiliki kuuza bidhaa iliyodhibitiwa chini ya Sheria;

“vifaa vya kitabibu” maana yake ni vifaa vinavyotumika kwa ajili ya kutibu, kurekebisha au kumhudumia mgonjwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya;

“viwanda vya kati” maana yake ni viwanda vyenye mtaji wa uwekezaji usio chini ya shilingi za kitanzania milioni mia mbili na usiozidi milioni mia nane;

“kuhakiki njia za uchunguzi” maana yake ni taratibu za kuthibitisha njia za uchunguzi za kimaabara ili kutoa majibu au matokeo yanayotarajiwa;

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya afya;

TS. Na. 412

“bidhaa zisizo za kitabibu” maana yake ni bidhaa zote isipokuwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa mujibu wa kanuni hizi;

“bidhaa zisizodhibitiwa” maana yake ni bidhaa nyingine isipokuwa bidhaa zinazodhibitiwa;

Sura 219

“dawa za magonjwa nadra” maana yake ni dawa zilizothibitishwa kwa mujibu wa Kanuni za Dawa za Magonjwa Nadra za mwaka 2018;

“ukaguzi wa awali” maana yake ni ukaguzi unaofanyika kabla ya utoaji wa leseni ili kuhakiki ukidhi wa masharti ya kisheria;

kibeba bidhaa" maana yake ni sanduku lolote, sehemu inayoweza kutenganishwa, tanki au kontena, kipokezi, au mpangilio wowote ambao bidhaa inaweza kubebwa;

“mfanyabiashara” maana yake ni mtengenezaji, mfungashaji, muingizaji, msafirishaji nje ya nchi, msambazaji, muuzaji au mfanyabiashara yoyote wa bidhaa zinazodhibitiwa chini ya Sheria;

“mfumo wa uhakiki ubora” maana yake ni njia, taratibu na michakato inayolenga kuhakikisha utoaji huduma bora kwa wateja ili kukidhi mahitaji yao;

"Cheti cha usajili" maana yake ni cheti kilichotolewa na Mamlaka kwa bidhaa au jengo iliyosajiliwa;

“bidhaa zinazodhibitiwa” maana yake ni dawa, vifaa tiba, vitendanishi, vifaa vya maabara na bidhaa za tumbaku;

“sampuli” maana yake ni sehemu ya bidhaa inayochukuliwa kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara kwa mujibu wa taratibu za uchukuaji sampuli;

“taratibu za uchukuaji sampuli” maana yake ni hatua zote zinazofuatwa wakati wa uchukuaji wa sampuli kwa kuzingatia takwimu za mzigo au toleo;

“viwanda vidogo” maana yake ni viwanda vyenye mtaji wa uwekezaji usiozidi shilingi za kitanzania milioni mia mbili;

“viwango vya upimaji” maana yake ni orodha ya vipimo, njia za uchunguzi na vigezo rejea ambavyo vinatoa wigo wa ukidhi wa bidhaa;

“bidhaa za tumbaku” maana yake ni majani, mabaki, sigara, siga na inajumuisha bidhaa nyingine za tumbaku zinazovutwa au kutafunwa kama na zinazotengezwa kwa kutumia tumbaku au mbadala wake; na

“miradi msonge” maana yake ni mpango wa taifa wa kudhibiti malaria,

UKIMWI, kifua kikuu na ukoma, chanjo na magonjwa yasiyopewa kipaumbele au magonjwa mengine yoyote kama yatakavyotambuliwa na Mamlaka.

## SEHEMU YA PILI
## ADA NA TOZO

Ada na tozo Sura ya 219

4.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kufanya biashara inayohusisha bidhaa zinazodhibitiwa chini ya Sheria, atawajibika kulipa ada na tozo kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mtu anaweza kuwasilisha sampuli za kibiashara kwa uchunguzi wa kimaabara na kulipa ada na tozo kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2), mtu anaweza kuwasilisha sampuli za bidhaa zisizodhibitiwa kwa uchunguzi wa kimaabara na kulipa ada na tozo kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3), huduma zingine zitakazotolewa na Mamlaka zitatozwa ada na tozo kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Nne.

(5) Ada na tozo zitalipwa kwa shilingi za Kitanzania au Dola za Kimarekani sawa na kiwango cha shilingi za Kitanzania au sarafu yoyote inayoweza kubadilishwa sawa na kiwango kinacholipwa kwa shilingi za kitanzania kwa tarehe ya malipo.

(6) Waziri anaweza, kwa ushauri wa Mkurugenzi Mkuu, kubadilisha ada na tozo zinazotumika wakati wowote.

(7) Mtu atakayechelewa kulipa ada na tozo chini ya kanuni hii atalipa ada na tozo husika pamoja na faini ya asilimia 15 ya ada na tozo aliyotakiwa kulipa.

Matumizi ya ada na tozo

**5.-** (1) Ada na tozo zitakazolipwa chini ya Kanuni hizi zitakusanywa na kutengwa kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka.

(2) Ada na tozo zitakazolipwa chini ya Kanuni hizi hazitarejeshwa.

(3) Mamlaka inaweza isitoe kibali cha uingizaji wa bidhaa nchini au kuongeza thamani ya mzigo endapo itajiridhisha kuwa thamani iliyoainishwa haiakisi uhalisia.

Kulipa kwa amri ya mahakama

**6 .-** (1) Endapo mahakama imetoa amri ya kumtaka mtu kulipa malimbikizo ya ada na tozo kwa bidhaa au huduma iliyotolewa na Mamlaka, malipo hayo yatajumuisha asilimia 15 ya jumla ya ada na tozo zilizopaswa kulipwa kabla ya amri ya mahakama.

(2) Tozo ya uingizaji wa bidhaa itapaswa kulipwa kabla ya usafirishaji wake.

Ada na tozo zilizoainishwa kwenye kanuni nyingine Sura ya 219

**7 .-** (1) Ada na tozo zilizoainishwa kwenye kanuni nyingine kwa mujibu wa Sheria, zitakuwa sehemu ya Kanuni hizi.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mtu ambaye atalipa ada na tozo chini ya kanuni nyingine zozote zilizotengenezwa chini ya Sheria, atachukuliwa kuwa amelipa ada na tozo kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Ada ya ukaguzi wa viwanda

**8 .-**(1) Ada ya ukaguzi wa viwanda vya dawa na vifaa tiba italipwa kwa kuzingatia mahali kiwanda kilipo.

(2) Mamlaka itatoza ada ya asilimia 25 ya gharama ya ukaguzi kwa kila njia ya ziada ya uzalishaji au kwa kila jengo la ziada lililoko ndani ya eneo la kiwanda.

Ada ya bidhaa za matangazo

**9.** (1) Bidhaa za matangazo zenye taarifa za kitabibu zitatozwa ada na tozo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), bidhaa za matangazo zambazo hazina taarifa za kitabibu hazitatozwa tozo.

Ada ya bidhaa za tumbaku

**10.** (1) Bidhaa za tumbaku zitatozwa ada na tozo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii bidhaa za tumbaku zitajumuisha sigara, siga, misokoto ya tumbaku, tumbaku ya kiko, tumbaku ya kutafuna na aina nyingine yeyote ya tumbaku inayovutwa.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA JUMLA

Makosa na adhabu

**11.** Mtu yeyote ambaye-

(a) Amekiuka au kushindwa kuzingatia Kanuni hizi; au

(b) Amesaidia mtu mwingine kutenda kosa, akipatikana na hatia, ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria.

Kufifilisha makosa

**12.-**(1) Mkurugenzi Mkuu, mkaguzi au mtu yeyote aliyeidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, endapo ameridhika kwamba mtu ametenda kosa anaweza kufifilisha makosa yake kwa kutoza kiasi cha jumla ya fedha kwa mujibu wa kosa husika.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), kiasi cha fedha kitakacholipwa kitakuwa mbili ya tatu ya jumla ya kiasi cha fedha ambacho kingelipwa kama faini ya kosa lililoainishwa katika Sheria.

(3) Mamlaka yaliyotolewa chini ya kanuni hii yatatekelezwa endapo mtuhumiwa atakiri kwamba ametenda kosa na kukubali kwa maandishi katika fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Tano kwa kosa ambalo limeshughulikiwa kwa mujibu wa kanuni hii.

(4) Mkurugenzi Mkuu, Mkaguzi au afisa yeyote aliyeidhinishwa wakati anatekeleza mamlaka kwa mujibu wa kanuni hii, atatoa risiti kwa kiasi cha fedha alichopokea chini ya kanuni ndogo ya (2).

(5) Kiasi cha fedha kitakachopokelewa chini ya kanuni hii kitalipwa kwa Mamlaka.

(6) Endapo shauri lolote litaletwa mahakamani dhidi ya mtu yeyote kwa makosa chini ya Kanuni hizi, itakuwa ni utetezi kama mtu huyo atathibitisha kwamba kosa analoshitakiwa limeshafifilishwa chini ya kanuni hii.

Kufutwa na kuhifadhi

**13.** (1) Kanuni za Ada na Tozo za Chakula, Dawa na Vipodozi za mwaka 2015 zinafutwa.

TS. Na, 464, 2015

(2) Ada na tozo zilizokusanywa au amri na hatua zote zilizochukuliwa chini ya

kanuni zilizofutwa kwenye kanuni ndogo ya (1), zitachukuliwa kuwa sehemu ya Kanuni hizi.

## MAJEDWALI

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

**ADA NA TOZO KWA BIDHAA ZINAZODHIBITIWA**

| NA. | HUDUMA | SARAFU | GHARAMA |
|---|---|---|---|
| | **DAWA** | | |
| | **Usajili wa Dawa za Binadamu na Mifugo (Zinazozalishwa ndani ya nchi)** | | |
| 1. | Ombi jipya au Kuhuisha usajili | TZS | 1,000,000 |
| 2. | Mabadiliko Makubwa | TZS | 200,000 |
| 3. | Mabadiliko Madogo | TZS | 100,000 |
| | **Usajili wa Dawa za Binadamu na Mifugo (Zinazozalishwa nje ya nchi)** | | |
| 4. | Ombi jipya au Kuhuisha usajili wa dawa zisizo za kibaiolojia | Dola za Marekani | 2,000 |
| 5. | Ombi jipya au Kuhuisha usajili wa dawa za kibaiolojia | Dola za Marekani | 3,000 |
| 6. | Kushikilia usajili | Dola za Marekani | 300 |
| 7. | Mabadiliko Makubwa | Dola za Marekani | 1,000 |
| 8. | Mabadiliko Madogo | Dola za Marekani | 300 |
| 9. | Usajili wa haraka | Dola za Marekani | Mara mbili ya ada husika |
| | **Bei elekezi ya dawa mpya** | | |
| 10. | Ombi jipya au kuhuisha | Dola za Marekani | 200 |
| | **VIFAA TIBA** | | |
| | **Usajili wa vifaa tiba (Vinavyotengenezwa nchini)** | | |
| 11. | Utambuzi wa vifaa tiba daraja A (Visivyohitaji usajili) | TZS | 50,000 |
| 12. | Daraja A (Vinavyohitaji usajili) | TZS | 100,000 |
| 13. | Daraja B | TZS | 200,000 |
| 14. | Daraja C | TZS | 500,000 |
| 15. | Daraja D | TZS | 500,000 |
| 16. | Mabadiliko makubwa | TZS | 150,000 |
| 17. | Mabadiliko madogo | TZS | 100,000 |
| | **Usajili wa vifaa tiba (Vinavyotengenezwa nje ya nchi)** | | |
| 18. | Utambuzi wa vifaa tiba daraja A (Visivyohitaji usajili) | Dola za Marekani | 100 |
| 19. | Daraja A (Vinavyohitaji usajili) | Dola za Marekani | 500 |
| 20. | Daraja B | Dola za Marekani | 2,000 |
| 21. | Daraja C | Dola za Marekani | 2,500 |
| 22. | Daraja D | Dola za Marekani | 2,500 |

| NA. | HUDUMA | SARAFU | GHARAMA |
|---|---|---|---|
| 23. | Vipuri na Vifaa vidogo | Dola za Marekani | 500 |
| 24. | Mabadiliko makubwa | Dola za Marekani | 300 |
| 25. | Mabadiliko madogo | Dola za Marekani | 150 |
| 26. | Kushikilia usajili (Vifaa tiba vilivyosajiliwa) | Dola za Marekani | 200 |
| 27. | Kushikilia usajili (Vifaa tiba vilivyotambuliwa) | Dola za Marekani | 50 |
| | **VITENDANISHI** | | |
| | **Usajili wa vitendanishi (Vinavyotengenezwa ndani ya nchi)** | | |
| 28. | Utambuzi wa vitendanishi daraja A (visivyohitaji usajili) | TZS | 50,000 |
| 29. | Daraja A (vinavyohitaji usajili) | TZS | 100,000 |
| 30. | Daraja B | TZS | 200,000 |
| 31. | Daraja C | TZS | 500,000 |
| 32. | Daraja D | TZS | 500,000 |
| 33. | Mabadiliko makubwa | TZS | 150,000 |
| 34. | Mabadiliko madogo | TZS | 100,000 |
| | **Usajili wa vitendanishi (Vinavyotengenezwa nje ya nchi)** | | |
| 35. | Utambuzi wa vitendanishi daraja A (visivyohitaji usajili) | Dola za Marekani | 100 |
| 36. | Daraja A (vinavyohitaji usajili) | Dola za Marekani | 300 |
| 37. | Daraja B | Dola za Marekani | 1,000 |
| 38. | Daraja C | Dola za Marekani | 1,500 |
| 39. | Daraja D | Dola za Marekani | 2,000 |
| 40. | Mabadiliko makubwa | Dola za Marekani | 500 |
| 41. | Mabadiliko madogo | Dola za Marekani | 200 |
| 42. | Kushikilia usajili (Vitendanishi vilivyosajiliwa) | Dola za Marekani | 200 |
| 43. | Kushikilia usajili (Vitendanishi vilivyotambuliwa) | Dola za Marekani | 50 |
| | **Tathmini ya ufanisi (Vitendanishi)** | | |
| 44. | Mashine ya kuchunguza hematolojia | Dola za Marekani | 3,000 |
| 45. | Mashine ya kuchunguza kemia ya damu | Dola za Marekani | 3,500 |
| 46. | Mashine ya kuchunguza molekyuli | Dola za Marekani | 5,300 |
| 47. | Mashine ya kuchunguza kemikali na molekyuli kwa teknolojia ya mwanga | Dola za Marekani | 5,300 |
| 49. | Mashine ya kubainisha mlolongo wa molekyuli | Dola za Marekani | 5,300 |
| 50. | Vitendanishi | Dola za Marekani | 3,000 |
| 51. | Kemikali za madoa, michanganyiko ya kuoteshea wadudu na diski | Dola za Marekani | 1,000 |

| NA. | HUDUMA | SARAFU | GHARAMA |
|---|---|---|---|
| 52. | Mashine ya kuchunguza bakteria | Dola za Marekani | 4,800 |
| **53.** | **Vitendanishi vingine** | | **3,000** |
| | **VIPUKUSI** | | |
| | **Usajili wa vipukusi (vinavyotengenezwa ndani ya nchi)** | | |
| 54. | Ombi jipya au la kuhuisha | TZS | 100,000 |
| 55. | Usajili wa vipukusi vinavyotengenezwa na viwanda vidogo na vya kati | TZS | 50,000 |
| | **Usajili wa vipukusi (vinavyotengenezwa nje ya nchi)** | | |
| 56. | Ombi jipya au la kuhuisha | Dola za Marekani | 300 |
| 57. | Mabadiliko | Dola za Marekani | 100 |
| 58. | Kushikilia usajili | Dola za Marekani | 80 |
| | **BIDHAA ZA TUMBAKU** | | |
| | **Usajili wa bidhaa za Tumbaku (zinazotengenezwa ndani ya nchi)** | | |
| 59. | Ombi jipya au la kuhuisha | TZS | 300,000 |
| 60. | Mabadiliko | TZS | 100,000 |
| 61. | Mabadiliko - madogo | TZS | 50,000 |
| | **Usajili wa bidhaa za Tumbaku (zinazotengenezwa nje ya nchi)** | | |
| 62. | Ombi jipya au la kuhuisha | Dola za Marekani | 300 |
| 63. | Mabadiliko - makubwa | Dola za Marekani | 100 |
| 64. | Mabadiliko - madogo | Dola za Marekani | 50 |
| | **MAJARIBIO YA DAWA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI** | | |
| 65. | Ombi la kufanya majaribio | Dola za Marekani | 3,000 |
| 66. | Mabadiliko makubwa ya majaribio | Dola za Marekani | 500 |
| 67. | Mabadiliko madogo ya majaribio | Dola za Marekani | 300 |
| 68. | Ombi la haraka | Dola za Marekani | Mara mbili ya gharama husika |
| | **UKAGUZI WA VIWANDA** | | |
| | **Ukaguzi wa viwanda vya dawa na vifaa tiba (Viwanda vya nje ya nchi)** | | |
| 69. | Afrika Mashariki | Dola za Marekani | 4,000 |
| 70. | Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) | Dola za Marekani | 4,500 |
| 71. | Nchi nyingine za Afrika | Dola za Marekani | 5,000 |
| 72. | Asia | Dola za Marekani | 6,000 |
| 73. | Ulaya | Dola za Marekani | 6,500 |
| 74. | Amerika | Dola za Marekani | 7,500 |
| 75. | Australia na New Zealand | Dola za Marekani | 7,500 |
| | **BIDHAA ZA MATANGAZO** | | |

| NA. | HUDUMA | SARAFU | GHARAMA |
|---|---|---|---|
| | **Tathmini na uidhinishaji wa Bidhaa za Matangazo** | | |
| | **Bidhaa za dawa** | | |
| 76. | Bidhaa za matangazo – dawa za ndani ya nchi | TZS | 100,000 |
| 77. | Tangazo lililofupishwa - ndani y nchi | TZS | 50,000 |
| 78. | Bidhaa za matangazo – dawa za nje ya nchi | Dola za Marekani | 100 |
| 79. | Tangazo lililofupishwa - dawa za nje ya nchi | | 50 |
| | **Bidhaa za tumbaku** | | |
| 80. | Ada ya udhibiti ya kila mwaka kwa wazalishaji, waagizaji na wauzaji wa jumla | TZS | 500,000 |
| | **VIBALI** | | |
| 81. | Kibali cha maonesho ya biashara-Kampuni ya kigeni | Dola za Marekani | 200 |
| 82. | Mabadiliko ya kampuni wakilishi | Dola za Marekani | 2,000 |
| 83. | Viwanda vikubwa vya dawa | TZS | 700,000 |
| 84. | Viwanda vya kati vya dawa | TZS | 500,000 |
| 85. | Viwanda vidogo vya dawa | TZS | 300,000 |
| 86. | Viwanda vikubwa vya vifaa tiba, vitendanishi na gesi tiba | TZS | 700,000 |
| 87. | Viwanda vya kati vya vifaa tiba, vitendanishi na gesi tiba | TZS | 500,000 |
| 88. | Viwanda vidogo vya vifaa tiba, vitendanishi na gesi tiba | TZS | 300,000 |
| 89. | Viwanda vikubwa vya vipukusi | TZS | 500,000 |
| 90. | Viwanda vya kati vya vipukusi | TZS | 300,000 |
| 91. | Viwanda vidogo vya vipukusi | TZS | 100,000 |
| 92. | Viwanda vikubwa vya bidhaa za tumbaku | TZS | 500,000 |
| 93. | Viwanda vya kati vya bidhaa za tumbaku | TZS | 300,000 |
| 94. | Waagizaji wa dawa nchini | TZS | 300,000 |
| 95. | Maghala ya waagizaji wa dawa nchini | TZS | 300,000 |
| 96. | Maduka ya jumla ya dawa za mifugo | TZS | 300,000 |
| 97. | Maduka ya jumla ya vifaa tiba | TZS | 300,000 |
| 98. | Maduka ya rejareja vifaa tiba | TZS | 100,000 |
| 99. | Maghala ya vifaa tiba na vitendanishi | TZS | 300,000 |
| 100 | Tozo ya kuteketeza mzigo uliokamatwa | TZS | 25% ya thamani ya mzigo |
| 101. | Ukaguzi wa shehena katika majengo ya wamiliki | TZS | 100,000 |
| | **Gharama za kuingiza mzigo** | | |
| 102. | Bidhaa za dawa | 2% ya thamani ya mzigo | |
| 103. | Vifaa tiba na vitendanishi | 2% ya thamani ya mzigo | |
| 104. | Vipukusi | 2% ya thamani ya mzigo | |
| 105. | Misaada ya dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vifaa vya maabara za kitabibu | 0.25% ya thamani ya mzigo | |
| 106. | Vifaa vya maabara za vituo vya kutolea huduma za afya | 2% ya thamani ya mzigo | |
| 107. | Vipuri na vifaa saidizi vya vifaa tiba, vitendanishi, na vifaa vya maabara za kitabibu | 0.5% ya thamani ya mzigo | |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 4(2))*

**SAMPULI ZA KIBIASHARA KWA AJILI YA UCHUNGUZI WA KIMAABARA**

| NA | VIPIMO | ADA TZS |
|---|---|---|
| | **DAWA** | |
| | **Vidonge, Kapsuli na Sacheti** | |
| 1. | Muonekano | 10,000 |
| | **Utambuzi wa viambata hai kwenye dawa** | |
| 2. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 150,000 |
| 3. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,000,000 |
| 4. | kwa kutumia mashine ya *FTIR* | 230,000 |
| 5. | kwa kutumia njia ya *TLC* | 300,000 |
| 6. | kwa kutumia njia ya mabadiliko ya rangi ya kikemikali | 180,000 |
| 7. | kwa ulinganisho wa kiwango cha jotoridi la myeyuko | 70,000 |
| 8. | kwa ulinganisho wa uwezo wa kupindisha mwanga | 70,000 |
| | **Kiwango cha viambata** | |
| 9. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 400,000 |
| 10. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,500,000 |
| 11. | Kwa kutumia njia ya *Titration* | 500,000 |
| 12. | kwa kutumia njia ya *Bioassay* | 400,000 |
| | **Kuyeyuka kwa vidonge na kapsuli** | |
| 13. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 300,000 |
| 14. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,600,000 |
| | **Uwiano wa viwango vya viambata hai kwenye dawa** | |
| 15. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 740,000 |
| 16. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 3,000,000 |
| 17. | kwa ulinganisho wa uzito | 60,000 |
| | **Vichafuzi** | |
| 18. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* (kiwango cha ukomo) | 1,200,000 |
| 19. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,500,000 |
| 20. | kwa kutumia njia ya *TLC* | 800,000 |
| 21. | kwa kutumia njia ya *TLC* (kiwango cha ukomo) | 150,000 |
| | **Masalia ya kemikali za majimaji** | |
| 22. | kwa kutumia mashine ya *GC/MS* | 1,500,000 |
| | **Kiwango cha unyevu** | |
| 23. | Kwa kutathmini tofauti ya uzito baada ya kukaushwa | 160,000 |
| 24. | kwa kutumia njia ya *Karl Fischer* | 1,000,000 |
| 25. | kwa kutumia njia ya *Titration* | 1,000,000 |
| 26. | kwa kutumia njia ya *Distillation* | 130,000 |
| | **Vipimo vingine** | |
| 27. | Kuvunjika kwa kidonge | 80,000 |
| 28. | Ugumu wa kidonge | 20,000 |
| 29. | Uwezo wa kidonge kustahimili kuvunjika | 60,000 |
| 30. | Kiwango cha *sulphate* kwenye majivu ya dawa | 530,000 |
| 31. | Madini tembo kwa kutumia mashine ya MPAES kwa kila madini | 100,000 |
| 32. | Utawanyiko wa kidonge kwenye maji | 80,000 |
| | **Vipimo vya Kimaikrobaiolojia** | |

| NA | VIPIMO | ADA TZS |
|---|---|---|
| 33. | Jumla ya vimelea hai vya bakteria na fangasi | 390,000 |
| 34. | Jumla ya vimelea vya ukungu na fangasi | 330,000 |
| 35. | Uwepo wa vimelea vya *Escherichia coli* | 280,000 |
| 36. | Uwepo wa vimelea vya *Pseudomonas aeruginosa* | 280,000 |
| 37. | Uwepo wa vimelea vya *Salmonella* | 350,000 |
| 38. | Uwepo wa vimelea vya *Staphylococcus aureus* | 350,000 |
| | **Dawa za maji** | |
| 39. | Muonekano | 10,000 |
| | **Utambuzi wa viambata hai** | |
| 40. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 150,000 |
| 41. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,000,000 |
| 42. | kwa kutumia mashine ya *FTIR* | 240,000 |
| 43. | kwa kutumia njia ya *TLC* | 400,000 |
| 44. | kwa kutumia njia ya mabadiliko ya rangi ya kikemikali | 180,000 |
| 45. | kwa ulinganisho wa uwezo wa kupindisha mwanga | 70,000 |
| | **Uchunguzi wa Kiwango cha viambata** | |
| 46. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 400,000 |
| 47. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,500,000 |
| 48. | Kwa kutumia njia ya *Titration* | 500,000 |
| 49. | kwa kutumia njia ya *Bioassay* | 400,000 |
| | **Uwiano wa viwango vya viambata hai kwenye dawa** | |
| 50. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 750,000 |
| 51. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 3,000,000 |
| 52. | kwa ulinganisho wa uzito | 60,000 |
| | **Vichafuzi** | |
| 53. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* (kiwango cha ukomo) | 1,200,000 |
| 54. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,500,000 |
| 55. | kwa kutumia njia ya *TLC* | 800,000 |
| 56. | kwa kutumia njia ya *TLC* (kiwango cha ukomo) | 140,000 |
| 57. | Ujazo wa dawa unaotoka | 60,000 |
| | **Masalia ya kemikali za majimaji** | |
| 58. | kwa kutumia mashine ya *GC/MS* | 1,500,000 |
| | **Kiwango cha unyevu** | |
| 59. | Kwa kutathmini tofauti ya uzito baada ya kukaushwa | 160,000 |
| 60. | kwa kutumia njia ya *Karl Fischer* | 1,000,000 |
| 61. | kwa kutumia njia ya *Titration* | 1,000,000 |
| 62. | kwa kutumia njia ya *Distillation* | 130,000 |
| | **Vipimo vya Kimaikrobaiolojia** | |
| 63. | Jumla ya vimelea hai vya bakteria na fangasi | 390,000 |
| 64. | Jumla ya vimelea vya ukungu na fangasi | 330,000 |
| 65. | Uwepo wa vimelea vya *Escherichia coli* | 280,000 |
| 66. | Uwepo wa vimelea vya *Pseudomonas aeruginosa* | 280,000 |
| 67. | Uwepo wa vimelea vya *Salmonella* | 350,000 |
| 68. | Uwepo wa vimelea vya *Staphylococcus aureus* | 350,000 |
| | **Vipimo vingine** | |
| 69. | Kiwango cha *sulphate* kwenye majivu ya dawa | 530,000 |
| 70. | Madini tembo kwa kutumia mashine ya MPAES kwa kila madini | 100,000 |
| 71. | Kiwango cha tindikali na alikali | 20,000 |
| 72. | Uzito wa kimiminika | 55,000 |

| NA | VIPIMO | ADA TZS |
|---|---|---|
| 73. | Kiwango cha *sulphate* kwenye majivu ya dawa | 530,000 |
| | **Dawa za sindano** | |
| 74. | Muonekano | 10,000 |
| | **Kiwango cha viambata hai** | |
| 75. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 400,000 |
| 76. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,500,000 |
| 77. | Madini kwa kutumia mashine ya MPAES kwa kila madini | 1,200,000 |
| 78. | kwa ulinganisho wa uwezo wa kupindisha mwanga | 70,000 |
| 79. | Kwa kutumia njia ya *Titration* | 500,000 |
| 80. | kwa kutumia njia ya *Bioassay* | 400,000 |
| | **Utambuzi wa viambata hai kwenye dawa** | |
| 81. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 150,000 |
| 82. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,000,000 |
| 83. | kwa kutumia mashine ya *FTIR* | 240,000 |
| 84. | kwa kutumia njia ya *TLC* | 400,000 |
| 85. | kwa kutumia njia ya mabadiliko ya rangi ya kikemikali | 180,000 |
| 86. | kwa ulinganisho wa uwezo wa kupindisha mwanga | 70,000 |
| | **Kiwango cha unyevu** | |
| 87. | Kwa kutathmini tofauti ya uzito baada ya kukaushwa | 160,000 |
| 88. | kwa kutumia njia ya *Karl Fischer* | 1,000,000 |
| 89. | kwa kutumia njia ya *Titration* | 1,000,000 |
| 90. | kwa kutumia njia ya *Distillation* | 120,000 |
| 91. | Kiwango cha tindikali na alikali | 20,000 |
| | **Vichafuzi** | |
| 92. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* (kiwango cha ukomo) | 1,200,000 |
| 93. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,500,000 |
| 94. | kwa kutumia njia ya *TLC* | 800,000 |
| 95. | kwa kutumia njia ya *TLC* (kiwango cha ukomo) | 140,000 |
| | **Masalia ya kemikali za majimaji** | |
| 96. | kwa kutumia mashine ya *GC/MS* | 1,500,000 |
| | **Uwiano wa viwango vya viambata hai kwenye dawa** | |
| 97. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 700,000 |
| 98. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 2,900,000 |
| 99. | kwa ulinganisho wa uzito | 60,000 |
| | **Vipimo vingine** | |
| 100. | Madini tembo kwa kutumia mashine ya MPAES kwa kila madini | 100,000 |
| 101. | Kiwango cha *sulphate* kwenye majivu ya dawa | 530,000 |
| 102. | Ujazo wa dawa unaotoka | 60,000 |
| 103. | Usafi wa kimiminika | 60,000 |
| 104. | Mabaki ya chembechembe kwenye dawa | 60,000 |
| 105. | Rangi ya kimiminika | 800,000 |
| 106. | Ujazo unaoweza kutolewa | 50,000 |
| | **Kutokuwepo kwa vimelea** | |
| 107. | Kwa kutumia njia ya *direct inoculation* au *membrane filtration* | 320,000 |
| 108. | Kwa kutumia njia ya *membrane filtration in closed system* | 350,000 |
| 109. | Kwa kuangalia uwepo wa *bacterial endotoxins* | 350,000 |
| | **Dawa za kupaka** | |
| 110. | Muonekano | 10,000 |
| | **Kiwango cha viambata** | |

| NA | VIPIMO | ADA TZS |
|---|---|---|
| 111. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 400,000 |
| 112. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,400,000 |
| 113. | Kwa kutumia njia ya *Titration* | 520,000 |
| 114. | kwa kutumia njia ya *Bioassay* | 400,000 |
| | **Utambuzi wa viambata hai** | |
| 115. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 150,000 |
| 116. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 1,000,000 |
| 117. | kwa kutumia mashine ya *FTIR* | 240,000 |
| 118. | kwa kutumia njia ya *TLC* | 400,000 |
| 119. | kwa kutumia njia ya mabadiliko ya rangi ya kikemikali | 180,000 |
| | **Uwiano wa viwango vya viambata hai kwenye dawa** | |
| 120. | kwa kutumia mashine ya *UV/VIS* | 750,000 |
| 121. | kwa kutumia mashine ya *HPLC* kwa kila kiambata hai | 3,000,000 |
| 122. | kwa ulinganisho wa uzito | 60,000 |
| | **Kiwango cha maji** | |
| 123. | kwa kutumia njia ya *Karl Fischer* | 1,000,000 |
